

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

*Anwani ya Simu: "REGCOM"
Simu ya mdomo: (028) 2220215-18
E-mail: ras.kagera@pmoralg.go.tz
Fax: (028) 2222341 / 2221356
Tovuti: www.kagera.go.tz*



**OFISI YA MKUU WA MKOA,
S. L. P. 299,
BUKOBWA - KAGERA.
TANZANIA.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
TAREHE 18 FEBRUARI, 2019**

**ZIARA YA MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB) WAZIRI MKUU WA
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MKOANI KAGERA
TAREHE 19 - 21 FEBRUARI, 2019**

Ndugu Waandishi wa Habari, Napenda nitumie fursa hii kuwataarifu Wananchi wa Mkoa wa Kagera kupidia Vyombo vya Habari Mkoani Kagera kuwa Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atafanya ziara ya Siku tatu hapa Mkoani kwetu Kagera kuanzia tarehe 19 Februari, 2019 hadi tarehe 21 Februari, 2019.

Ndugu Waandishi wa Habari, Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatarajia kuwasili Mkoani kwetu tarehe 19/02/2019 siku ya Jumanne saa 6:00 Mchana kupidia Wilaya ya Biharamulo. Mhe. Waziri Mkuu mara baada ya kuwasili Mkoani Kagera Wilayani Biharamulo atatembelea na kukagua kituo cha afya Nyakanazi ambacho kimejengwa na baadhi ya majengo kukarabatiwa kwa shilingi milioni 500 zilizotolewa na Serikali Kuu. Mara baada ya kutembelea na kukagua kituo cha Afya Nyakanazi Mhe. Waziri Mkuu ataongea na Wananchi wa Wilaya ya Biharamulo na Mkoa wa Kagera kwa ujumla katika mukutano wa hadhara katika uwanja wa Shule ya Msingi Nyakanazi.

Ndugu Waandishi wa Habari, Tarehe 20/02/2019 Mhe. Waziri Mkuu ataendelea na ziara yake Wilayani Karagwe na Missenyi ambako atafanya shughuli za Chama. Aidha, tarehe 21/02/2019 Mhe. Waziri Mkuu ataendelea na ziara yake Wilayani Bukoba ambako atatembelea na kukagua miradi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) pamoja na kufanya shughuli za Chama na kuhitimisha ziara yake ya siku tatu Mkoani Kagera siku hiyo ambapo ataondoka majira ya 10:20 jioni kuelekea Dodoma.

Ndugu Waandishi wa Habari, Nawaomba wananchi wa Mkoa wa Kagera kuonesha ushirikiano, bashasha na ukarimu kwa Mhe. Waziri Mkuu kwa kufika kwa wingi katika maeneo yaliyotajwa hasa Wilayani Biharamulo atakakoingilia mkoani kwetu ili kumpokea na kumkaribisha katika kwetu Kagera. Vilevile Wilaya zote atakazopita au kutembelea Mhe. Waziri Mkuu za Muleba, Bukoba (Bukoba Manispaa), Missenyi na Karagwe wananchi wanahamasishwa kujitokeza kwa wingi kumpokea na kumuonesha ukarimu na wetu sisi Wanakagera.

Aidha, natoa wito kwa wananchi kudumisha umoja, amani na mshikamano wakati wote wa ziara ya Mhe. Waziri Mkuu na kutojihuisha na vitendo vyta uhalifu au uvunjifu wa amani kwani Vyombo vyetu vyta Ulinzi na Usalama vipti tayari muda wote kushughulika na wananchi wasiopenda amani. Aidha, kama ilivyo kawaida na desturi ya wananchi wa Mkoa wa Kagera kudumisha usafi wa mazingira tunaomba kuendelea kudumisha utamaduni huo ili kuweka maeneo yetu katika hali ya usafi tunapompokea kiongozi wetu wa kitaifa.

Kagera, Kazi Amani na Maendeleo.
Kazi Amani na Maendeleo, Kagera

Imetolewa na; Mhe. Brigedia Jenerali Marco E. Gaguti
Mkuu wa Mkoa
KAGERA